

**HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA MHE. SAADA MKUYA SALUM
(MB.) KATIKA UZINDUZI NA USAMBAZAJI WA TAKWIMU ZA
PATO LA TAIFA ZILIZOREKEBISHWA KWA MWAKA WA KIZIO
WA 2007 TANZANIA BARA, TAREHE 19 DESEMBA, 2014
UKUMBI WA KARIMJEE - DAR ES SALAAM**

Ndugu Mwenyekiti;

Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa;

Wawakilishi wa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali;

Wawakilishi kutoka Taasisi za Elimu ya Juu na Utafiti;

Wawakilishi kutoka Sekta Binafsi;

Ndugu Wanahabari;

Mabibi na Mabwana.

Ndugu Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru waandaaji wa hafla kwa kunikaribisha kuja kuzindua na kusambaza rasmi matokeo ya Takwimu za Pato la Taifa zilizorekebisha kwa Tanzania Bara. Uzinduzi huu unahitimisha kazi kubwa ya marekebisho ya takwimu za Pato la Taifa uliyofanywa tangu mwaka 2011. Aidha, uzinduzi kama huu utafanyika Tanzania Zanzibar mwezi Januari, 2015.

Ndugu Mwenyekiti na Washiriki wengine, madhumuni makuu ya uzinduzi huu ni kutangaza rasmi mabadiliko ya kiashiria muhimu cha uchumi jumla ambacho ni takwimu za Pato la Taifa zilizorekebishwa kwa kutumia bei za bidhaa na huduma za mwaka 2007 ili kuendana na hali ya maendeleo ya kiuchumi duniani. Aidha, kama tunavyofahamu takwimu rasmi za Pato la Taifa ni miongoni mwa viashiria vya uchumi jumla duniani ambazo hutumika katika kupanga na kutathmini mipango na program mbalimbali za maendeleo ya Wananchi, hivyo ni wito wangu kwa maafisa mipango na wadau wengine kutumia takwimu hizi katika kupanga mipango ya maendeleo ya wananchi wetu.

Ndugu Mwenyekiti, Tanzania inaungana na Nchi nyingine duniani katika kuboresha takwimu za Pato la Taifa ambapo kazi ya kurekebisha takwimu za Pato la Taifa ilianza tangu mwaka 2011. Marekebisho haya ya takwimu za Pato la Taifa kwa Tanzania Bara yalianza mara baada ya uhuru mwaka 1966 ambapo tulitumia Mfumo wa Kimataifa wa Kutayarisha takwimu za Pato la Taifa wa mwaka 1953. Aidha, tumeendelea kufanya maboresho mbalimbali kulingana na miongozo inayotolewa na Umoja wa Mataifa, ambapo maboresho ya sasa ni ya tano na yametumia Mfumo wa Umoja wa Mataifa wa mwaka 1993 na 2008.

Ndugu Washiriki wetu, kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, napenda kutangaza kwamba matokeo ya takwimu za Pato la Taifa zilizorekebishwa zinaonyesha kuwa, Pato la Taifa kwa mwaka 2007 lilikuwa shilingi trilioni 26.8 ikilinganishwa na shilingi trilioni 20.9 ambazo ni takwimu za Pato la Taifa zilizokuwa zinatumia bei za bidhaa na huduma za mwaka 2001. Hii ni sawa na ongezeko la ukubwa wa Pato la Taifa kwa kiasi cha asilimia 27.8. Aidha, Wastani wa Pato la Mwananchi mwaka 2013 kwa kutumia takwimu za Pato la Taifa zilizorekebishwa ni Shilingi 1,561,050/= ambazo ni sawa na Dola za Kimarekani 977 ikilinganishwa na Sh. 1,186,200/= ambazo ni sawa na Dola za Kimarekani 742 kwa kutumia takwimu za Pato la Taifa za bei ya mwaka 2001.

Ndugu Mwenyekiti na Washiriki, ukubwa wa Pato la Taifa ni matokeo ya juhudi za Serikali za kutengeneza fursa kwa Wananchi za kukuza uchumi wa Mwananchi mmoja mmoja. Naomba nifafanue kuwa kuongezeka kwa Pato la Taifa haina maana kuwa Serikali ina uwezo wa kuwajaza Wananchi fedha mifukoni mwao bila ya wao kufanya kazi, bali ni kuwapatia fursa za kufanya kazi za kujiajiri na hatimaye kupata kipato halali kutokana na kazi walizofanya.

Ndugu Mwenyekiti na Washiriki, tumeona kuwa ukubwa na uchumi wetu umechangia na kujumuishwa kwa shughuli ambazo zimeibuka hivi karibuni, ikiwa ni pamoja na kukua kwa sayansi na teknolojia. Kwa mujibu ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, zaidi ya asilimia 63 ya wananchi wa Tanzania Bara wanamiliki simu za kiganjani, hivyo kutokana na kukua huku kwa sayansi na teknolojia, kumetoa fursa muhimu kwa wananchi kujiongezea kipato. Utumiaji wa simu ya kiganjani unamwezesha mwananchi kurahisisha mawasiliano kutafuta masoko ya bidhaa ndani na nje ya nchi, pamoja na kukamilisha miamala mbalimbali ya kibenki na mikopo, hivyo kuongezeka kwa huduma hii kuongeza ajira, kupunguza misururu mirefu katika mabenki, hivyo muda huo kutumika katika uzalishaji wa shughuli zingine.

Hata hivyo, kuongezeka kwa thamani ya Pato la Taifa kunaiongezea Serikali uwezo wa kimapato kupitia kodi na hivyo kugharamia ujenzi wa miundombinu na utoaji wa huduma mbalimbali kwa Wananchi. Aidha, naomba ikumbukwe kwamba Pato la Taifa ni Jumla ya thamani itokanayo na mchango wa Mwananchi mmoja mmoja, Ushirika wa Wananchi, Makampuni, Serikali na Sekta Binafsi.

Kwa mfano thamani ya nyanya za mkulima wa kijiji cha Ilula inajumuishwa na thamani ya nyanya zilizozalishwa sehemu nyingine nchini na kuwa thamani ya zao la nyanya katika Pato la Taifa. Hata hivyo, zao la nyanya linatoa ajira kwa wakulima, wasafirishaji, wachuuzi na hatimaye mlaji wa mwisho anapata huduma hiyo. Mfano huu wa nyanya unahusu vilevile bidhaa na huduma zote katika uchumi hapa Nchini.

Ndugu Mwenyekiti na Washiriki, Serikali na Sekta Binafsi zimeweza kuongeza ajira mpya zipatazo 400,000 kati ya 600,000 zilizokuwa zinatarajiwa kupatikana katika sekta iliyo rasmi. Sanjari na upatikanaji wa ajira hizo, huduma za upatikanaji wa maji safi na salama zimeendelea kuimarika kama ilivyoainishwa katika Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi ya mwaka 2012; ambapo zaidi ya asilimia 60 ya Kaya zote nchini zinapata huduma ya maji safi na salama hususan maeneo ya mjini. Aidha, kwa mujibu wa matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 yanaonyesha kwamba, zaidi ya asilimia 20 ya kaya zote nchini zinatumia nishati ya umeme kwa kuangazia. Haya ni baadhi ya matokeo ya fursa ya ukuaji wa uchumi ambao umepelekea umaskini wa kipato kupungua kutoka asilimia 35 mwaka 2007 hadi asilimia 28.2 mwaka 2012.

Ndugu Mwenyekiti, baadhi ya nchi ambazo zimeshafanya marekebisho ya takwimu za Pato la Taifa ni pamoja na Ghana na Nigeria. Kwa upande wa nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, Uganda imefanya marekebisho kutoka bei za mwaka 2002 na kuwa bei za mwaka 2009/10 na matokeo yalikuwa ni kuongezeka kwa Pato la Taifa kwa asilimia 17.5, Kenya kutoka bei za mwaka 2001 na kuwa bei za mwaka 2009 na matokeo yalikuwa ni kuongezeka kwa Pato la Taifa kwa asilimia 20.5, Rwanda kutoka bei za mwaka 2009 na kuwa bei za mwaka 2011 na matokeo yalikuwa ni kuongezeka kwa Pato la Taifa kwa asilimia moja.

Ndugu Mwenyekiti na washiriki, pamoja na matumizi ya takwimu hizi Kimataifa, program za maendeleo hapa nchini, kama vile Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini II (MKUKUTA II), Dira ya Taifa ya mwaka 2025, Mpango wa Miaka Mitano ya Maendeleo 2011 – 2016, Changamoto za Maendeleo za Milenia 2015 na Matokeo Makubwa Sasa takwimu hizi zitatumika katika kutathmini malengo yaliyowekwa kwa ajili ya kuboresha zaidi maisha ya Wananchi.

Ndugu Mwenyekiti, kabla ya kumaliza napenda kutambua mchango mkubwa wa Mashirika ya Maendeleo ya Uingereza na Canada pamoja na Benki ya Dunia kupitia Mpango Kabambe wa

Kuboresha na Kuimarisha Takwimu Nchini (Tanzania Statistical Master Plan - TSMP) kwa kugharamia zoezi hili. Vilevile, Serikali inatambua msaada wa kiufundi wa utayarishaji wa takwimu za Pato la Taifa zilizorekebisha kutoka Ofisi ya Takwimu ya Denmark na Shirika la Fedha Duniani. Ninashukuru Wizara, Idara na Taasisi mbalimbali za Serikali zilizoshirikiana na Wizara yangu na hatimaye kukamilisha kazi hii muhimu kwa ajili ya Taifa letu.

Ndugu Mwenyekiti, Serikali pia inatambua jukumu kubwa linalotekelezwa na Wanahabari la kuelimisha umma kwa lengo la kujenga uelewa miongoni mwa wananchi kuhusu manufaa ya marekebisho ya takwimu za Pato la Taifa. Hivyo, niwaombe kwa mara nyingine tena kuwa mafunzo mtakayoyapata muyatumie vema katika kuelimisha umma kuhusu matumizi ya takwimu hizi. Sambamba na hili, napenda kutoa wito wangu kwa wadau wote kutumia takwimu hizi rasmi katika kupanga mipango ya maendeleo ya kiuchumi kwa Taifa.

Ndugu Mwenyekiti, Mabibi na Mbwana, baada ya maelezo hayo, napenda kutamka rasmi kuwa; **"TAKWIMU ZA PATO LA TAIFA ZILIZOREKEBISHWA KWA KUTUMIA BEI ZA MWAKA 2007 ZIMEZINDULIWA RASMI"**.